

**OFISI YA TAIFA YA USALAMA SERIKALINI WAKABIDHI KITABU CHA MWONGOZO
WA KANUNI ZA USALAMA SERIKALINI KWA KATIBU MKUU KIONGOZI – DODOMA
10 JANUARI, 2020**

Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Mhandisi John W. H. Kijazi, leo tarehe 10 Januari, 2020 amekabidhiwa Kitabu cha Mwongozo wa Kanuni za Usalama Serikalini, na Bwana Mululi M. Mahendeka ambaye ni Afisa Usalama wa Serikali. Muongozo huo umeandaliwa na Ofisi ya Taifa ya Usalama Serikalini, makabidhiano hayo yamefanyika ofisini kwa Katibu Mkuu Kiongozi, Ikulu ya Chamwino, Wilayani Chamwino, Mkoani Dodoma.

Akikabidhi kitabu hicho, Bw. Mahendeka alisema zoezi la kukabidhi nakala za kitabu hicho kwa watendaji wakuu wa serikali litafanyika kwenye ofisi zote za serikali zilizopo Makao Makuu ya Serikali Mkoani Dodoma pamoja na mikoa mingine yote nchini. Aidha, alibainisha kuwa kitabu hiki kilichopigwa chapa na Mpigachapa Mkuu wa Serikali, ni toleo la mwaka 1999 ambalo limefanyiwa maboresho mwaka jana 2019 ili kuendana na mabadiliko mbalimbali yaliyopo katika utendaji kazi Serikalini na utekelezaji wa kanuni za usalama Serikalini.

Vitabu hivi ukabidhiwa kwa watendaji Wakuu wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya pamoja na Watendaji wa Serikali katika Halmashauri na Serikali za Mitaa.

Miongoni mwa kanuni za kiusalama zilizopo katika mwongozo huo ni, usalama wa taarifa na nyaraka za Serikali, usalama wa majengo ya serikali na usalama na matumizi sahihi ya vifaa vya TEHAMA. Vilevile katika kanuni hizo kuna vipengele vinavyosisitiza Watumishi wa Umma kupewa elimu ya usalama, kufanyiwa upekuzi wa kiusalama (vetting), kula kiapo cha kutunza siri za Serikali kwa mujibu wa Sheria Namba 3 ya Usalama wa Nchi ya mwaka 1970. Pia kanuni hizo zinabainisha hatua zinazostahili kuchukuliwa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma kwa mtumishi au watumishi watakaokiuka kanuni husika.

Naye Katibu Mkuu Kiongozi alitoa maelekezo kwa Ofisi ya Usalama Serikalini, kuongeza nguvu katika kutoa elimu na mafunzo ya mara kwa mara kuhusu kanuni za usalama Serikalini kwa watumishi wa Umma wa ngazi zote, ili waweze kuzielewa na kuzifuata kikamilifu katika utendaji wao wa kazi wa kila siku kwa faida ya Serikali na Taifa kwa ujumla.